# JARIDA LA MANISPAA YA KINONDONI

ISSN2507-8797X Toleo Maalum No 1, 2024/2025

## HONGERA KINONDONI KWA USHINDI NANENANE








# “KUMBUKIZI” YA MATUKIO MBALIMBALI YA MAONESHO YA NANENANE 2023

**Picha mbalimbali zikionesha matukio ya maonesho ya Nanenane Mwaka 2023 katika banda la Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni yaliyofanyika Mkoani Morogoro Ambapo Manispaa ya Kinondoni iliibuka kuwa mshindi wa tatu kwa Mkoa wa Dar es Salaam kwa Mwaka 2024 Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi imejipanga vizuri kuonesha na kutoa elimu kwa Wananchi juu ya kilimo mjini, ufugaji na uvuvi wa kisasa ili kuongeza hali ya afya na lishe safi kwa Wananchi.**


















# KINONDONI IMEJIPANGA VIZURI MAONESHO NANENANE 2024




**MHARIRI MKUU**
*Aquilinus Shiduki*

**MHARIRI MSAIDIZI**
*Beatha Singano*

**WAPIGA PICHA**
*Kaunga Maulid*
*Filbert Odilo*

**MSANIFU JARIDA**
*Kaunga Maulid*

**WAANDISHI**
*Kaunga Maulid*
*Hadija Mgeni*
*Mathias Msabila*
*Jovine Mutabuzi*
*Joely Obadia*
*Kumbuka Malogo*

*JARIDA HILI LIMETOLEWA NA*
*KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI*
*HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI*
*S. L. P, KINONDONI, 31902 DSM*
*SIMU: +255222170173*
*BARUA PEPE: md@kinondonimc.go.tz*

***Chagua Viongozi Bora wa Serikali za Mitaa kwa Maendeleo Endelevu ya Kilimo, Mifugo wna Uvuvi”*** hii ni kauli mbiu katika maonesho ya nanenane mwaka 2024 ambapo Manispaa ya Kinondoni ilifanikiwa kuibuka mshindi wa kwanza kwa kanda ya Mashariki na kwa Mkoa wa Dar es Salaam.

Katika tuzo hizo zilizotolewa na Waziri Mkuu Mstaafu Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda katika siku ya ufungaji wa maonesho hayo yaliyofanyika Mkoani Morogoro Manispaa ya Kinondoni ilifanikiwa kuwa mshindi wa kwanza kwa ubora wa vipando kwa kanda nzima ya Mashariki katika maonesho hayo.

Ikumbukwe kuwa maonesho ya Nanenane Kanda ya Mashariki 2024 yamefanyika Mkoani Morogoro ikihusisha Mikoa minne ikiwepo Mkoa wa Dar es Salaam, Pwani, Tanga na Mkoa wa Morogoro ikiwa mwenyeji ya maonesho hayo.

w

# TAHARIRI

## KILIMO MJINI CHAIPAISHA KINONDONI MAONESHO YA NANENANE 2024



*Picha zikionesha tuzo mbili walizo pata Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kwenye maonesho ya nanenane yaliyofanyika Mkoani Morogoro ikiibuka mshindi wa kwanza kwa Kanda ya Mashariki na mshindi wa kwanza kwa Mkoa wa Dar es salaam.*

MAONESHO YA NANENANE kwa mwaka 2024 yamekuwa ya aina yake kwa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni. Maonesho hayo yaliyoanza Agosti Mosi na kuhitimishwa Agosti 08, 2024 na Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, yaliiibua Manispaa ya Kinondoni katika ushindi wa jumla kwa kanda ya Mashariki na ushindi kwanza kwa halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam.

Manispaa imeweza kushiriki maonesho hayo kwa kushirikisha wadau wake kutoka vikundi mbalimbali vya wajasiriamali katika sekta za usindikaji mazao, ufumaji wa nguo, wafugaji, wakulima na wavuvi. Aidha kupitia maonesho hayo, Manispaa iliweza kuwasilisha kwa wananchi namna bora ya kutekeleza Kilimo Mjini.

Kwa Manispaa ya Kinondoni, maonesho ya Nanenane ya mwaka huu yalizingatia kutangaza vipaumbele vya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan. Vipaumbele hivyo ni Kutekeleza Mkataba wa Lishe; Nishati safi ya kupikia na Kilimo chenye tija. Wataalamu wa Manispaa walifafanua kwa weledi mkubwa vipaumbele hivi kwa kuhusianisha na dhana nzima ya manonesho hayo.

Kwa upande wa Kilimo, vipando vya mbogamboga, matunda na vyakula mbalimbali viliweza kutafsiri dhana ya Kilimo Mjini ambapo Mkulima anaweza kutumia eneo dogo kuzalisha mazao kwa wingi na hivyo kuwa na kilimo chenye tija. Aidha, uwepo wa bwawa la Samaki na mabanda ya mifugo kama Ng’ombe, Kuku, Bata, wanyama wadogo wadogo, kulitafsiri pia dhana ya ufugaji bora, wenye tija na unaozalisha mahitaji ya vyakula kwa ajili ya Lishe bora na ukuaji.

Kwa upande mwingine, washiriki wa maonesho kupitia Manispaa ya Kinondoni waliweza kutafsiri dhana ya uwezeshwaji wananchi kiuchumi kupitia mikopo ya asilimia Kumi. Kupitia maonesho hayo, washiriki walipata fursa ya kuuza bidhaa zao, kuunganishwa na masoko lakini pia kutangaza bidhaa zao.

Ni matumaini yetu kuwa, kupitia maonesho hayo, Sisi kama Manispaa tumepata fursa ya kujifunza na kufundisha wananchi na washiriki wengine waliofika katika maonesho hayo dhana ya Kilimo Mjini. Ni matumaini yetu sasa, tutayaona matokeo ya maonesho hayo katika mitaa yetu 106 iliyopo Manisaa ya Kinondoni. Tukutane Nanenane 2025.

# VIJANA WASHAURIWA KUJIKITA KWENYE KILIMO, MIFUGO NA UVUVI

**Na**
**JOVIN MUTABUZI**

Waziri Mkuu Mstaafu wa Tanzania Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda amewataka vijana kutambua umuhimu wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi katika kukuza maendeleo ya taifa na kipato cha mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Pinda ameyasema hayo wakati akifunga maonesho ya nanenane yaliyofanyika Mkoani Morogoro Agost 8, 2024 ambapo Manispaa ya Kinondoni ilifanikiwa kutwaa tuzo mbili kwa kuwa mshindi wa kwanza kwa Kanda ya Mashariki na Mkoa wa Dar es Salaam.

“Ikiwa leo ni siku ya mwisho ya maonesho haya kwa mwaka huu 2024 niwaombe Wananchi hasa vijana kwa ujumla kujikita au kujiajiri kwenye kilimo kwani kilimo ni moja ya ajira kubwa kwa vijana ambao wamekuwa wakihangaika na ajira,” alisema Mhe. Pinda.

Aidha, Mheshimiwa Pinda ameitaka Kamati ya Maandalizi ya maonesho hayo Kanda ya Mashariki kuweka utaratibu wa kuwatembelea wakulima hao kwenye Manispaa zao ili kuakisi kile



*Waziri Mkuu Mstaafu Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda akiwa kwenye ufungaji wa maonesho ya nanenane ya mwaka 2024 yaliyofanyika Mkoani Morogoro kwa Kanda Mashariki ikijumuisha Mikoa minne Dar es Salaam, Pwani, Tanga na Morogoro.*

kinachooneshwa hapo kiwe dhahiri ndani ya Manispaa hizo.

Mbali na hayo pia Mheshimiwa Pinda amesema kuwa maonesho ya nanenane kwa mwaka 2024 yaliyofanyika Mkoani Morogoro ndio maonesho bora kati ya maonesho yote yaliyofanyika hapa nchini, hivyo niwapongeze Wakulima, Wavuvi na Wafugaji kwa maonesho hayo.

Maonesho ya nanenane yamejumuisha Mikoa minne ikiwepo Mkoa wa Dar es Salaam, Tanga, Pwani na Morogoro.







# MAFUTA YA MCHAICHAI YAFANYA VIZURI MAONESHO YA NANENANE

**Na HADIJA MGENI**

Mafuta ya Mchaichai ni moja ya bidhaa zilizoonekana kuwa na mvuto mkubwa kwenye maonesho ya naenane yaliyofanyika Mkoani Morogoro kwa Kanda ya Mashariki.

Kwa kanda ya Mashariki yalijumuisha mikoa Minne ikiwepo Mkoa wa Dar es Salaam, pwani, Tanga na Mkoa wa Morogoro ambao ndio mwenyeji wa maeonesho hayo.

Akiongea katika maonesho hayo Mjasiriamali wa bidhaa za virutubisho lishe na viungo vya vyakula kutoka Vijimambo Group Bi. Grace Calist amesema kuwa mafuta ya mchaichai yanafukuza mbu, wadudu warukao na watambaao hivyo ni bidhaa bora na yenye faida kubwa kwa binadamu.

"Kiukweli bidhaa zetu ni bora na ni nzuri mnoo kwani zimekuwa na matokeo chanya kwa watumiaji wangu wote wanaotumia dawa hizi hasa mafuta haya ya mcahichai nwengi wamekuwa wakipiga simu kurudisha majibu kwangu hivyo niwaombe wananchi kuchamgamkia fursa hii ya matumizi ya mafuta ya mchaichai kutokana na faida zake," alisema Bi. Grace.



*Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni Mheshimiwa Saad Mtambule (kulia) akiwa na mjasiriamali kutoka bidhaa za Vijimambo Bi. Grace Msimbe kwenye maonesho ya Nanenane Mkoani Morogoro.*

Aidha, Bi. Grace ameishauri jamii kuwa na desturi ya kutumia mchaichai kwenye matumizi mbalimbali ya nyumbani hasa kufukiza moshi wake ndani ya nyumba ili kuleta harufu nzuri na kuondoa mambo mabaya ndani ya nyumba.

Bi. Grace ameishukuru Manispaa ya Kinondoni kwa kuona umuhimu wa kumpeleka kwenye maonesho ya nanenane ili kuonesha bidhaa zake mbalimbali ikiwepo mafuta ya Mchaichai, mafuta ya Mwarobaini na dawa nyingine lukuki.

Mbali na mafuta hayo pia Bi. Grace amesema kuna mafuta ya muarobaini yanayondoa fangasi za ndani na nje, muwasho usioisha na wakati mwengine harara tu au kama visunzua ambayo unapaka tu vinapotea kabisa.

Lakini kwa watoto wenye mapunye au ana madoa sehemu fulani dawa hiyo imekuwa ikifanya vizuri sana, pia kinaponesha vidonda sugu aidha ni cha oparesheni au cha sukari akitumia mafuta hayo ni mazuri na yanaponesha kwa haraka.

Kuna bidhaa ya Anti- age( unga wa majani ya mstafeli) tengeneza juisi kunywa glasi moja asubuhi na jioni moja sio lazima kila siku hata kwa wiki mara moja inasaidia kuamsha seli zilizosinyaa kuwa hai ina madini ya zink, protein na calcium ya kutosha.

Mafuta ya Amra yana faida nyingi, ikiwa unatumia kama kinga haina masharti ila ukitumia kama dozi mfano una matatizo ya mifupa, calcium imepungua mwilini, ukitembea magoti yanasagana ukienda hospitali unaambiwa ute ute umeisha. Tengeneza kama uji au maji kunywa inasaidia kuongeza ute uliopungua kwenye magoti unaweza kutumia. .hadi siku kumi na nne kwa kipimo cha kijiko cha chai.





# ELIMU YA KILIMO MJINI KUWAFIKIA WANANCHI KINONDONI

Na
**KAUNGA MAULID**




Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni Mheshimiwa Saad Mtambule amewaomba Maafisa Kilimo, Mifugo na Uvuvi pamoja na wadau wa kilimo, mifugo na uvuvi kutumia utaalam wao kuwafikia watu wengi ili waweze kijikwamua kimaisha na kiuchumi.

Mheshimiwa Mtambule ameyasema hao August 5, 2024 baada ya kutembelea banda la Manispaa ya Kinondoni kwenye maonesho ya nanenane yanayoendelea Mkoan Morogoro yenye kauli mbiu isemayo "Chagua Viongozi Bora wa Serikali za Mitaa kwa Maendeleo Endelevu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi,".

"Kwanza niwapongeze sana kwa maandalizi mazuri ya vipando vizuri na vinavyofutia, lakini niwaombe tutue utaalamu na elimu hii kufakia watu wengi zaidi ndani ya Wilaya ya Kinondoni na ikiwezekana tusambaze elimu na teknolojia hizi za kitaalamu nchi nzima," alisema Mhe Mtambule.



Aidha, Mkuu wa Wilaya huyo ameitaka Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kufanya tathimini ya haraka mara baada ya kumalizika kwa maonesho hayo ya nanenane ili kuweza kujipanga vizuri kwa maonesho yajayo ya mwaka 2025 kwa kushirikisha wadau mbalimbali wa kilimo, mifugo wa uvuvi ili kuimarisha zaidi sekta hiyo.

Hata hivyo Mheshimiwa Mtambule amewapongeza wadau hao waliopo ndani ya banda la Manispaa ya Kinondoni kwa kuonesha ubunifu wa hali juu katika uzalishaji wa bidhaa mbalimbali za vyakula ambavyo vinasaidia katika uboreshaji wa vyakula hasa kwa watoto wenye umri chini ya miaka 10 ambao ndio wako kwenye hatari kubwa ya kukosa lishe bora kutokana na mtindo wa maisha ndani ya jamii.



# WADAU WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI WAKARIBISHWA MALOLO

**Na**
**HADIJA MGENI**



*Wadau mbalimbali wa wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi wakitembelea banda la manispaa ya Kinondoni kwenye maonesho ya nanenane 2024 yaliyofanyika Mkoani Morogoro.*

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kupitia Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi inawakaribisha wadau wa kilimo, mifugo na uvuvi kuja kujifunza kwenye kituo cha mafunzo Malolo kilichopo Mabwepande.

Hayo yamebainishwa na Mkuu wa Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi Manispaa ya Kinondoni Bi. Kulwa Mkwama akiwa kwenye maonesho ya nanenane yaliyofanyika Mkoani Morogoro mwaka huu 2024.

“ Katika kituo chetu tunatoa teknolojia mbalimbali kwa wakulima ambao wanatutembelea kituoni. Tuna mashamba mablimbali ya kilimo ambayo tunafanya kilimo cha matango, mboga mboga, uyoga pia tunafanya bidhaa za keki pamoja na mikate.

Kwa upande wake Afisa kilimo Hamza Mpota kutoka kituo cha kilimo Malolo amesema Kituo hiki kinafanya kazi na wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi kama mnavyoona niko na mtaalam kutoka Japan ametuletea teknolojia ya uzalishaji wa matango kwa kutumia mbinu ya kisasa ambayo inatoa matango bora kama unavyoona, lakini pia tunazalisha mabilinganyi yenye ubora mkubwa ambayo wakulima wetu wakiyafatilia wana uwezo wa kupata mapato mazuri sana. Tunawakaribisha sana katika kituo cha Malolo ili waje kujifunza.



# KINONDONI YATOA TAHADHARI KWA WAKULIMA

**Na MWANDISHI WETU**

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kupitia Divisheni ya Mipango na Takwimu imewataka Wakulima kuchukua tahadhari dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi kwa kujikita katika kilimo kinachoendana na mabadiliko hayo.

Hayo yamebainbishwa na Mchumi na Mratibu wa Maafa Manispaa ya Kinondoni Bw. Bakar Mlanzi wakati akiwa katika mafunzo kwa Wakulima juu ya namna ya kukabiliana na maafa ambayo yanasababishwa na mabadiliko ya tabia ya nchi.

“Kwasasa kumekuwa na mbadiliko makubwa sana hivyo ni muhimu sana kwa wakulima kutumia mafunzo haya kwa kutumia mafunzo haya kukabiliana na athari hizi za mabadiliko ya tabia ya nchi hasa kipinmdi hiki cha mvua zinazoendelea kunyesha, hivyo amewataka wakulima hao kukabiliana na madilliko ya tabia nchi kwa kuanzisha vikundi vitakavyowawezesha kuanzisha kilimo kitachohimili mabadiliko ya tabia ya nchi sambamba na kushiriki katika mafunzo mbalimbali ya kilimo ili kuleta teja katika kilimo," alisema Bw. Bakari.

Aidha Bw. Bakari alisema kuwa kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi na mvua zinazoendelea kunyesha wakulima wanatakiwa kukabiliana na madilliko hayo kwa kuhifadhi mazao kutokana mvua kuwa nyingi ambayo imapelekea kuharibu mazao shambani na kusababisha upungufu wa chakula.

Mafunzo hayo yaliyoandaliwa na Divisheni ya Kilmo, Mifugo na Uvuviyalitolewa katika Kituo cha Mafunzo ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi Malolo kilichopo Mabwepande, Manispaa ya Kinondoni.



*Moja ya picha za mbogamboga zinazolimwa ndani ya Manispaa ya Kinondoni katika kituo cha kutolea mafunzo ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi Malolo kilichopo Kata ya Mabwepande Manispaa ya Kinondoni.*

***Tufatilie kwenye mitandao yetu ya kijamii Instagram, Twitter, Facebook, WhatSap, TikTok kwa Kina la “kinondonimunicipal” na Youtube KMC MEDIA***

# KINONDONI YATOA ELIMU YA KILIMO CHA VANILA MAONESHO YA NANENANE

**Na**
**CATHERINE MSHANI**

Manispaa ya Kinondoni iliyatumia Maonesho ya nanenane Kanda ya Mashariki yaliyofanyika Mkoani Morogoro ikijumuisha Mikoa ya Dar es salaam, Morogoro, Tanga na Pwani kutoa elimu ya namna ya kunufaika na kilimo cha zao la Vanila hususani kwa Wakulima wanaojishughulisha na kilimo cha mjini.

Elimu hiyo ilitolewa na Wataalam pamoja na Wakulima wanaojishughulisha na kilimo cha zao hilo walioletwa na Manispaa ya Kinondoni kwaajili ya kuonesha bidhaa za mazao hayo na utoaji wa elimu ya kuhusiana na kilimo chake sanjari na manufaa yake.

Frank Mstapha ambaye ni mtalaamu wa kilimo cha vanila, anasema kuwa, Vanila ni zao ambalo linatumia miaka miwili mpaka mitatu kufikia ukomavu wake, eneo nzuri linalotakiwa ili zao la Vanila lishamili vilivyo linatakiwa kuwa na joto la wasitani na pia linahitaji kivuli kwa asilimia 50, alisema Bw. Frank.



*Mtalaamu wa Kilimo cha Vanila kutoka Manispaa ya Kinondoni Bw. Frank Mstapha akitoa maelezo mafupi kwa Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni Mhe. Saad Mtambule na Mkuu wa Divisheni ya ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi Bi. Kulwa Mkwam kwenye maonesho ya nanenane yaliyofanyika Mkoani Morogoro.*

Aidha, Bw Frank alisema kuwa, wakulima na Watu mbalimbali wanaohitaji kujifunza zaidi juu ya zao la vanila watembelee katika maeneo yetu ya vipando hata baada ya Maonesho haya ya nanenane tutaendelea kuwapa elimu zaidi.

"Tunawakaribisha wote wenye kiu ya kutaka kujifunza kuhusu zao hili, ukifika utapata maelezo kwa undani zaidi namna ambavyo utaweza kupata miche yake, na namna ya kuipanda mpaka kuweza kufikia hatua ya ukomavu hatimaye uweze kuipeleka sokoni". aliongeza Bw Frank.



# WAFUGAJI WAPASWA KUTUMIA NJIA YA UHIMILISHAJI ILI KUWA NA MIFUGO BORA




*Banda la malisho ya Ng'ombe kwenye maonesho ya nanenane yaliyofanyika Mkoani Morogoro 2024 ikionesha hatua mbalimbali za uhimilishaji wa Ng'ombe kwa njia ya kisasa na bora zaidi.*

**Na**
**KUMBUKA MALOGO**

Uhimilishaji ni upandishaji wa ng'ombe kwa njia ya chupa, ambapo kwa kutumia teknolojia hii mfugaji anaweza kupata mazao bora ya nyama au maziwa kutoka kwa wanyama wanaozaliwa au kuzalishwa.

Akielezea kuhusu umhimu na faida ya teknolojia hii, Mtalaamu wa Uhimilishaji kutoka Manispaa ya Kinondoni Ndg Emmanuel Thomas, alisema kuwa,

Uhimilishaji unampa mfugaji faida na nafasi ya kuchagua aina ya mnyama anayemtaka pia gharama zake ni ndogo tofauti na njia za asili zilizoeleka.

" Njia hii inarahisisha katika utunzaji wa kumbukumbu pamoja na kwamba mfugaji anaweza kuwa na mifugo michache lakini anazalisha mazao ya kutosha,

mfugaji anaepusha gharama za kufuga dume ambapo kutunza dume mmoja kwa mwaka mzima unaweza ukajikuta umetumia zaidi ya laki mbili mpaka laki tatu kwa ajili ya tiba na malisho". aliongeza Ndg Thomas.

Kadhalika, Ndg Thomas ameendelea kuwashauri Wafugaji hususani wale wa mjini kutumia njia ya Uhimilishaji ili kuendana na Sera na Sheria za ufagaji Mjini ili waende sambamba na utaratibu utakiwao pia wapate matunda stahiki yenye ubora madhubuti.



# ZAO LA KARANGA LAFANYA VIZURI NANENANE MOROGORO

**Na**
**MATHIAS MSABILA**



Mikopo ya asilimia kumi (10%) yaongeza thamani ya bidhaa za karanga kutoka kikundi cha akina mama cha Farmers Market kilichopo Oysterbay Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni.

Akiongea kwa niaba ya kikundi hicho Bi. Sophia Achimwede amesema kuwa mikopo ya asili kumi imewasaidia kwa kiasi kikubwa kikundi chao katika kukuza mitaji na kuongeza thamani ya biashara zao za karanga.

"Bidhaa yetu inapatikana kwa bei za jumla na rejareja kwaajili ya kuwapa vipato wajasiliamali wadogo ambao hawana uwezo wa kupata mashine.

Sisi tumewezeshwa kwa asilimia kumi (10%) na Mama Samia mpaka kufikia kupata mashine za kusindika karanga. Kwahiyo tunawaribisha wateja wetu tunatuma mzigo ndani na nje ya nchi," alisema Bi. Sophia.



Bi. Sophia ameongeza kuwa Farmers Market wanasindika unga ambao unatokana na zao la karanga ambalo bado linaendeleza mnyororo wake ndani ya nchi yetu ikiwa unga huu ni unga halisi wa karanga unaotumika kama kiungo kwa kuunga kwenye supu, mboga au uji kwa matumizi ya chakula.

Mbali na hayo pia Bi. Sophia amesema kuwa Farmers Market inasindika pilipili ambayo inachakata kwa kutumia zao la pilipili ambalo linalimwa ndani ya Manispaa ya Kinondoni. Tunachukua kwa wakulima na kuiongeza thamani mwisho wa siku inakua mezani tayari kwa kuliwa.

"Hii ni vinegar ambayo ni kiungo cha kumarineti nyama ya kuku, ng'ombe au samaki. Ina ndimu, limao na kitunguu swaumu. Tumeitengeneza wenyewe kwa kusindika na kuongeza thamani mpaka hapa ilipo,' alisema Bi. Sophia.

Pia Bi. Sophia amesema kuwa wana viungo vya chai, pilau na mboga, vyote hivyo vinapatikana ndani ya Manispaa ya Kinondoni kupitia taasisi yetu Swahili Farmers Market.

Aidha, Bi. Sophia ameishukuru Serikali kupitia Manispaa ya Kinondoni kwa kuwawezesha mikopo ya asilimia 10 wajasiriamali wadogowadogo kama kikundi chao ambapo inasaidia kuongeza vipato, mitaji na thamani ya bidhaa zao ili kuendana na soko la ushindani.



"Chagua Viongozi Bora wa Serikali za Mitaa kwa Maendeleo Endelevu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi"

# BANDA LA MANISPAA YA KINONDONI KWENYE MAONESHO YA NANENANE












# MATUKIO MBALIMBALI KATIKA PICHA



*Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni Mheshimiwa Saad Mtambule akiwa akiwa kwenye maonesho ya nanenane Mkoani Morogoro banda la Manispaa ya Kinondoni akiangalia namna bora bora na njia ya ukaushaji wa Samaki kwa kutumia kaushio la Samaki linalitumia nishati ya jua na chumchi.*



*Meya wa Manispaa ya Kinondoni na Diwani wa Kata ya Mwananyamala Mhe. Songoro Mnyonge akitembelea bidhaa mbalimbali za kilimo, mifugo na uvuvi zilizopo banda la Manispaa ya Kinondoni kwenye maonesho ya nanenane 2024 kwa yaliyofanyika Mkoani Morogoro kwa Kanda ya Mashariki*



*Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni Bi. Hanifa Suleiman Hamza eya wa (katikati) akiakibeba kombe la ushindi baada ya kuibuka mshindi wa kwanza kwa kanda ya Mashariki na kwa Mkoa wa Dar es Salaam kwenye maonesho ya nanenane yaliyofanyika Mkoani Morogoro kwa kanda ya Mahariki ambapo inajumuisha Mikoa minne Dar es Salaam, pwani. Tanga na Morogoro.*




*Wataalamu na Wadau wa kilimo, mifugo na uvuvi kutoka Manispaa ya Kinondoni washishangilia ushindi wa nafasi ya kwanza pamoja na Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni Bi. Hanifa Suleiman Hamza (katikati) kwenye ,aonesho ya nanenane 2024 kwa kanda ya Mashariki na kwa Mkoa wa Dar es Salaam.*



*Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni Bi. Hanifa Suleiman Hamza akiipongeza Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi sambamba na wataalam wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi kutoka Mnaispaa ya Kinondoni kwa kufanikisha ushindi mnono kwenye maonesho ya nanenane 2024 mara baada kupokea tuzo hizo.*



*Picha ikionesha makombe mawili ya ushindi uliopatika kwenye maonesho ya naenane yaliyofanyika Mkoani Morogoro (kulia) ni kombe la mshindi wa kwanza kwa kanda ya Mashariki na kusho ni kombe la mshindi wa kwanza kwa Mkoa wa Dar es Salaam.*



"Chagua Viongozi Bora wa Serikali za Mitaa kwa Maendeleo Endelevu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi"



# SWAHILI FARMER’S YATOA ELIMU YA USAFISHAJI MFUMO WA UPUMUAJI

**Na**
**JOELY OBADIA**



Swahili Farmers Market yatoa elimu juu ya namna ya uboreshaji wa bidhaa za mimea zinazosaidia usafishaji wa mfumo wa upumuaji, urembo na usindikaji wa viungo mbalimbali vya chai.

Elimu hiyo imetolewa na Mjasiriamali kutoka Swahili Farmers Market Bi. Farida Nassor akiwa kwenye maonesho ya nanenane yaliyofanyika Mkoani Morogoro ambapo Manispaa ya Kinondoni ilifanikiwa kuwa mshindi wa kwanza kwenye maonesho hayo kwa Kanda ya Mashariki.

Akiongea kwenye maonesho hayo Bi. Farida amesema kuwa Swahili Farmers Market Cooperative ni chama cha ushirika ambacho kinajishughulisha na utengenezaji wa dawa za mimea zinazotokana na kilimo, ufugaji na uvuvi.

“Kutokana na kauli mbiu yetu ya mwaka huu inasema “chagua viongozi bora serikali ya mtaa kwa maenendeleo endelevu ya ufugaji mifugo na uvuvi” hivyo

sisi kama Swahili Farmers Market tumejikita katika bidhaa hizi za kilimo, ufugaji na uvuvi ili kuisaidia jamii hasa katika magonjwa yote yatokanayo na mfumo wa upumuaji,” alisema Bi. Farida.

Mbali na hayo pia Bi. Farida amesema kuwa Swahili Farmers Market inatengeneza bidhaa mbalimbali za urembo ambapo bidhaa hizo zinatengenzwa kutokana na mimea aina mbalimbali ya inayolimwa kwenye mashamba.

Aidha, Bi Farida amesema kuwa kuna bidhaa inaitwa Dead Sea Mud Soap ni sabuni ambayo imetengenezwa kwa tope la bahari lililokufa ambayo inachanganywa na viungo vya mbogamboga kama nyanya, karoti na matunda. sabuni hii ni kwaajili ya magonjwa ya ngozi yaliyoshindikana kama fangasi, mabarango na mashilingi.

Kuna bidhaa inaitwa hii bidhaa inaitwa Allanblackia Butter, ni bidhaa ambayo imeipandishwa thamani kutoka kwenye zao la mbegu ya mmea huo na kuwa mafuta kwaajili ya ngozi, nywele, kuondoa mabaka, mabarango, weusi na mikunjo ya ngozi kiasili zaidi.

Bi. Farida ameongeza kuwa Swahili Farmers Market tuna hii hidhaa ya Lemon Grass Oil ni mafuta ya mchaichai ya asili yakiyochanganywa na Shea butter, mafuta ya nazi, zaituni na Algan oil. Kazi yake kubwa ni kusafisha mfumo wa ngozi, kufukuza mbu, kufanya masaji, maumivu




ya viungo vya mwili.

Pia tuna mafuta ya Mnyonyo ambayo tunakamua wenyewe kwaajili ya kufanyia masaji, magonjwa ya ngozi, kuondoa harara na miwasho kwani mafuta hayo yanatayarishwa kwa kukamuliwa vizuri na hayajachanganywa na kitu chochote.

Sambamba na mafuta hayo pia kuna mafuta ya Chebe hair growth ni mafuta ya nywele yenye mchanganyiko wa mafuta mbalimbali ikiwemo Allanblackia Butter, Shea na Mango butter. Imechanganywa kwa pamoja na viambaupishi mbalimbali vya mafuta ya asili ya mimea ikiwa kazi yake ni kukuza, kufanya nywele isikatike na kufanya nywele ibaki na weusi wake wa asili.

”Tuna bidhaa ya Aloe Vera Gel kwaajili ya ngozi na nywele kwa kufanya steaming na kuchanganya viambaupishi kama mayai, asali kwaajili ya nywele. Pia inatumika kama scrub kwa kuchanganya viambaupishi kama kahawa, manjano na liwa kutumia kama Facial Wash( kusafisha uso)”.

HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI INAWASHUKURU WADAU WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI KWA USHIRIKIANO NA MCHANGO WAO KATIKA KUFANIKISHA USHINDI WA KWANZA KWENYE MAONESHO YA NANENANE AMBAPO MANISPAA YA KINONDONI ILIIBUKA MSHINDI WA KWANZA KWA KANDA YA MASHARIKI NA KWA MKOA WA DAR ES SALAAM

**ASANTENI SANA**

# TIMU YA WATUMISHI MANISPAA YA KINONDONI IKIJIANDAA NA SHIMISEMITA 2024









# PICHA MBALIMBALI ZA MAONESHO YA NANENANE MOROGORO















# JARIDA LA MANISPAA YA
# KINONDONI



**Mhe. SAAD MTAMBULE**
**Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni**

**Bi. STELLA MSOFE**
**Katibu Tawala wa Wilaya ya Kinondoni**

**Mhe. SONGORO MNYONGE**
**Meya Manispaa ya Kinondoni**

**Bi. HANIFA SULEIMAN HAMZA**
**Mkurugenzi Manispaa ya Kinondoni**